**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA**
*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)*

Simu:0232935443
Barua pepe: **td@nanyambatc.go.tz**

S.L.P 1490,
**NANYAMBA-MTWARA.**

Tarehe: **09/07/2023**

---

# TANGAZO LA KUPATA VIKUNDI/MAFUNDI (LOCAL FUNDI) KWA AJILI YA UJENZI WA SHULE MPYA YA SEKONDARI KATIKA KATA YA MTINIKO.

## (MRADI WA SEQUIP)

## A. MAJENGO YATAKAYOJENGWA KATIKA SHULE YA KATA MTINIKO.

**1) UJENZI WA MADARASA MAWILI (02)**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/01 Lot 1

**2) UJENZI WA MADARASA MAWILI (02)**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/01 Lot 2

**3) UJENZI WA MADARASA MAWILI (02) NA OFISI MMOJA (01)**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/01 Lot 3

**4) UJENZI WA MADARASA MAWILI (02) NA OFISI MMOJA (01)**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/01 Lot 4

**5) UJENZI WA JENGO LA UTAWALA**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/02

**6) UJENZI WA MAABARA YA KEMIA NA BIOLOJIA**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/ Mtiniko SS/2022/2023/W/102/03

**7) UJENZI WA MAABARA YA FIZIKIA**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/04

8) **UJENZI WA MAKTABA**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/05

9) **UJENZI WA CHUMBA CHA TEHAMA**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/06

10) **UJENZI WA MATUNDU 08 YA VYOO**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/07

11) **UJENZI WA KICHOMEA**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/08

12) **UJENZI WA TANKI LA MAJI LA ARDHINI**

- KAZI NA: LGA/178/HQ/GVT/Mtiniko SS/2022/2023/W/102/09

Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kupitia **OR-TAMISEMI** imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa **Vyumba vya Madarasa, Jengo la Utawala, Maabara, Maktaba, Chumba Cha Tehama, Kichomea taka, Matenki ya Maji na Matundu ya Vyoo kwaajili ya Shule Mpya ya Kata ya Mtiniko** katika Halmashauri ya Mji Nanyamba Kupitia Mradi wa **SEQUIP**. Aidha, Halmashauri ya Mji imepokea fedha hizo kwa ajili ya ujenzi huo kwa maelekezo ya kutumia utaratibu wa **'Force Account'** ili kazi itekelezwe kwa wakati.

Hivyo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtimbwilimbwi kwa Niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Nanyamba anawatangazia Vikundi/Mafundi wa fani mbalimbali, wenye nia na uwezo wa kutekeleza kazi zilizooneshwa hapo juu kwa ubora na viwango vinavyokubalika.

**MASHARTI KWA MWOMBAJI:**

1. Awe na uzoefu wa kazi za ujenzi zinazofanana na kazi zilizooneshwa kwa kuambatisha **Orodha ya Kazi zote na Gharama (CV)** alizowahi kufanya tangu aanze kufanya kazi za Ufundi Uashi ikiwemo mawasiliano ya alikowahi fanya kazi au mkataba.

2. Tangazo hili linatolewa kwa muda wa **siku saba (07)** tangu tarehe **09/07/2023** hadi tarehe **18/07/2023** na kuwa muda wa utekelezaji wa ujenzi wa mradi huu utakuwa muda wa siku/wiki/miezi **(fundi ajaze kwenye barua ya maombi)** tangu siku ya kusaini mkataba.

3. Kampuni yoyote ya kikandarasi **haitaruhusiwa** kuleta maombi ya kazi hizi.

4. Vikundi watakaoomba kazi hii watapewa kipaumbele zaidi. Pia, waoneshe uzoefu katika kazi za ujenzi wa majengo ya serikali Kiambatisho ni kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha (1) cha tangazo hili.

5. Kazi zitakazo fanyika ni ujenzi wa **Vyumba vya Madarasa na Matundu.**

6. Vifaa vyote vya ujenzi (Building Materials) vitatolewa na Mwajiri. Fundi atalipwa gharama ya kazi tu **(Labour Charge)** kwa siku/wiki/mwezi kulingana na makubaliano.

7. Fundi awasilishe uthibitisho wa kutokuwa ametenda kosa la kijinai, kuwa na mgogoro na Serikali.

8. Fundi awe na kitambulisho cha **NIDA** au **MPIGA KURA** au barua kutoka kwa mtendaji wa Mtaa/Kijiji/Kata.

9. Fundi atatakiwa kuonesha uthibitisho wa kuwa na **vitendea kazi** muhimu vitakavyo mwezesha kukamilisha kazi husika (Mfano:- Pima Maji, Mwiko, Ndoo, Karai, Ngazi, Birigi (Plumb Bob), Water Level, Nyundo Ndogo Za Mawe, Chepe (Spade), kamba ya manila za kunyoshea na kuseti na vinginevyo.

10. Fundi atatakiwa kuonesha uthibitisho wa kuwa na Vifaa vya Kuvaa wakati wa Shughuli za Ujenzi kwaajili ya Usalama wakati wa Kazi **Mfano, Kofia Ngumu, Gloves, Viatu vya Kufunika, Reflector n.k**

11. Vikundi/Mafundi wa fani mbalimbali, wenye nia na uwezo wa kutekeleza kazi zilizooneshwa hapo juu kwa **ubora na viwango** vinavyokubalika, wanaweza kuainisha kazi **moja au Zaidi**.

12. Kabrasha linaloonesha Vyumba vya madarasa, Jengo la Utawala, Maabara, Maktaba, Chumba cha TEHAMA na Matundu ya vyoo pamoja na fomu mbalimbali zinapatikana katika Ofisi Mkuu wa Shule Mtimbwilimbwi kuanzia tarehe **09/07/2023** hadi tarehe **18/07/2023** kuanzia saa **1.30 asubuhi** hadi saa **9.30 Alasiri**. Katika **Ofisi ya Mkuu wa Shule Mtimbwilimbwi sekondari.**

13. Maombi ya kazi ya ufundi yaandikwe kwa herufi kubwa yakionesha aina ya kazi uliyoomba, Jina la fundi au Kikundi na yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro wala alama yoyote na yafungwe kwa lakili. Aidha, bahasha ifungwe vizuri. Pia, juu ya **bahasha iandikwe Jina la kazi uliyoomba na Jina La Shule**. Namba ya kazi husika na anuani ya:

    **Mkuu wa Shule,**
    **Shule ya Sekondari Mtimbwilimbwi,**
    **S. L. P. 1490,**
    **NANYAMBA.**

14. Maombi yote katika nakala **halisi moja (1)** iwekwe ndani ya bahasha moja (1) na **nakala (copy) mbili (2)** yawekwe kwenye bahasha moja (1) kisha bahasha mbili ziwekwe kwenye bahasha moja kubwa na yaletwe kwenye ofisi ya Mkuu wa Shule ya Sekondari Mtimbwilimbwi kuanzia **saa 1.30** asubuhi hadi saa **9.30 Alasiri.**

15. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi hayo ni tarehe **18/07/2023** saa **4.30 asubuhi** na maombi hayo yatafunguliwa hadharani mara tu, baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha.

16. Kabrasha la maombi ya kazi ya ujenzi wa majengo tajwa hapo juu linapatikana kwa **Tzs. 20,000.00** katika ofisi ya Mkurugenzi wa Mji iliyopo katika Halmashauri ya Mji Nanyamba. Hakikisha unapewa risiti mara baada ya malipo.

17. Maombi yote ya kazi za ufundi yatakayowasilishwa baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha hayatapokelewa.

18. Siku ya kutembelea eneo la mradi ili kuwezesha kujaza makabrasha itakuwa tarehe **14/07/2023** siku ya **Ijumaa** katika eneo la Mradi iliyopo **kijiji cha Mtiniko** husika kuanzia **saa 4:30 asubuhi**. Gharama za kutembelea eneo la mradi kila mwombaji atajitegemea.

19. Mwajiri anaweza kufuta maombi yote ya zabuni bila taarifa, ikiwa kutakuwa na sababu ya kufanya hivyo kwa maslahi mapana ya wananchi, Halmashauri na Serikali kwa ujumla.

20. Waombaji wote wanaombwa kuhudhuria katika ufunguzi wa kazi hii **Tarehe 18/07/2023 katika Shule ya Sekondari Mtimbwilimbwi saa 4:30 Asubuhi.**

MOHAMED MWISHEHE MOHAMED
Mkuu Wa Shule
**MTIMBWILIMBWI SEKONDARI**